

Bw. Philipo Chandy

Bw. Philipo Chandy alizaliwa tarehe 21 Machi, 1965 Rorya Mkoani Mara. Bw. Chandy alisoma shule ya msingi Bitiryo, Rorya Mkoani Mara (1977-1983) na elimu ya Sekondari katika shule ya Sekondari Ihungo (1984-1987) mkoani Kagera. Bw. Chandy alipata elimu ya juu ya Sekondari katika shule ya Sekondari Mwenge (1988-1990) iliyopo mkoani Singida.

Kati ya mwaka 1991-1995, Bw. Chandy alihudhuria mafunzo Chuo Kikuu cha Kilimo Sokoine na kutunukiwa Shahada ya Sayansi ya Chakula na Teknolojia. Bw. Chandy ana Shahada ya Uzamili katika Sayansi ya Mazingira kutoka Chuo Kikuu cha Dar es Salaam aliyotunukiwa mwaka 2001.

Kabla ya kujiunga na Utumishi wa Umma mwaka 2006, Bw. Chandy alikuwa Afisa Uchakataji na Uhakiki Ubora katika kiwanda cha mafuta cha Tradeco, New Tradeco *Investment* (2000) Ltd na kiwanda cha Maji ya chupa cha Masafi.

Bw. Chandy aliteuliwa na Katibu Mkuu Wizara ya Maji kwenye nafasi ya Mkurugenzi Msaidizi aliyekuwa anashughulikia Ushauri wa Kitaalam na Utafiti katika masuala ya Ubora wa Maji. Novemba, 2018 aliteuliwa kukaimu nafasi ya Mkurugenzi wa Ubora wa Maji akichukua nafasi iliyoachwa na Inj. Nadhifa S. Kemikimba ambaye ni Mkurugenzi wa Idara ya Usambazaji wa Maji na Usafi wa Mazingira Wizara ya Maji.